# JARIDA LA SIKONGE DC

TOLEO NA. 5

OKTOBA - DESEMBA 2023

SIKONGE HAKUNA KILICHO SIMAMA



KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI - HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE



# KAMATI YA SIASA WILAYA YA SIKONGE YAPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CHAMA CHA MAPINDUZI 2020 – 2025.

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge DC.

Kamati ya Siasa Wilaya ya Sikonge imeketi leo kwa ajili ya kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2023 katika ukumbi wa CCM Wilaya ya Sikonge.

Mhe. Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Simon Chacha akiwasilisha taarifa hiyo amesema utekelezaji wa ilani ya uchaguzi inatekelezwa vizuri ukiondoa dosari ndogondogo zinazorekebishika na kikubwa ni kudumisha uhusiano mzuri kati ya chama na Serikali ili kufikia malengo.

Kwa upande wake Bi. Anna Chambala,Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sikonge akifunga kikao hicho baada ya wajumbe kuijadili na kuipokea taarifa hiyo amesema “Taarifa ni nzuri,Hongera sana Mhe. DC,mapungufu yaliyopo ni ya kawaida,Ushauri wetu uzingatiwe”.



# WATUMISHI SIKONGE WAPATIWA MAFUNZO YA MFUMO MPYA WA MANUNUZI YA UMMA KWA NJIA YA MTANDAO.(NeST).

Na. Robert Magaka.

Mafunzo hayo yametolewa leo katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge yakiongozwa na wataalam toka vitengo na divisheni mbalimbali waliohudhuria mafunzo hayo ya mfumo mpya wa manunuzi katika ngazi ya mkoa.

Akitoa mada katika mafunzo hayo Kaimu mkuu wa kitengo cha Usimamizi wa Manunuzi na Ugavi Bw. Revocatus Shaban amesema mfumo huu mpya wa NeST utasaidia kudhibiti rushwa na uwazi usioridhisha katika mchakato wa zabuni serikalini pamoja na kupunguza matumizi ya karatasi nyingi katika ujazajaji wa fomu mbalimbali wakati wa mchakato wa manunuzi.

Lakini pia mfumo huu mpya wa manunuzi ya umma kwa njia ya mtandao (NeST) utasadia kutatua changamoto zilizojitokeza katika mfumo wa zamani wa manunuzi wa TANePS,ambao ulianza kutumika mwezi Januari 1,2020.

Kuanzia tarehe 1 Oktoba manunuzi yote ya umma yatafanyika kupitia mfumo mpya wa NeST.NeST itasimamia usajili,zabuni,mikataba,malipo,katalogi pamoja na minada kwa njia ya mtandao.



# “LENGO LETU KUBWA NI HILO KUHUDUMIA WATU”.DED PANDAWE.

Na. Robert Magaka - Sikonge.

Hayo yamesemwa leo katika kikao cha watumishi wa Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge na Mkurugenzi Mtendaji Ndg. Selemani Pandawe alipokuwa akiongea na watumishi hao katika ukumbi wa halmashauri.

Aidha watumishi hao wakiwasilisha kero kwa Mwenyekiti wa kikao hicho ndugu Pandawe,wamelalamikia kutofanyika kwa vikao vya idara na divisheni katika maeneo yao hivyo kuleta sintofahamu ya mambo mengi ambayo kwa kufanyika vikao hivyo yangepatiwa majibu na kupunguza au kuondoa kabisa kero hizo.

Naye Mwenyekiti akijibu juu ya kero hiyo iliyoonekana kuwa ya jumla amesema Wakuu wa Divisheni na Vitengo wanapaswa kukaa vikao na watumishi wao kila mwezi kati ya tarehe 20 hadi 30 na mihtasari ya vikao hivyo iwasilishwe kwa Afisa Utumishi kwa ajili ya ufuatiliaji.

Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu, Ndg. Nico Kayange amesisitiza juu ya watumishi wa umma kuzingatia sheria na kanuni za utumishi hasa katika suala zima la mavazi, kwa kuvaa nguo zenye staha na nadhifu.

Akifunga kikao hicho Ndg. Pandawe amesisitiza watumishi wote kuzingatia sheria kila mtu katika eneo lake lakini pia kutunza siri za serikali wanazopata kuzifahamu kulingana na majukumu yao ya kila siku.



# MHE. DC CHACHA AONGOZA BARAZA LA BIASHARA LA WILAYA YA SIKONGE.

Na. Robert Magaka - Sikonge.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. Simon Chacha ameongoza kikao cha baraza la biashara katika ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge leo tarehe 10 Septemba,2023.
Akifungua baraza hilo amesema mapato mengi ya Serikali yanatokana na shughuli za watu wanazofanya,hivyo mazingira ya kufanya shughuli hizo yanapaswa kuwa mazingira mazuri ili kuwasaidia wananchi wafanye shughuli zao kwa amani.

Katika baraza hilo wajumbe wamechangia sababu mbalimbali zinazo zorotesha sekta ya biashara,viwanda na uwekezaji ikiwemo utambuaji wa mazingira halisi ya uwekezaji pamoja na kuchelewa kwa kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki kufunguliwa.

Akijibu changamoto hizo Bwana Peter Mpeta Mkuu wa Idara ya Viwanda na Uwekezaji amesema Halmashauri ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha ujazwaji wa mkataba na mzabuni Ngoda Traders ili kiwanda kianze uzalishaji rasmi na kwa upande wa maeneo ya uwekezaji Mpeta amesema kuwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya uwekezaji hayatabadilishwa hivyo wawekezaji wawe huru kuendelea na uwekezaji hasa katika maeneo ya Stendi Kuu ya Mabasi pamoja na eneo la maegesho ya magari ya mizigo.



Aidha akichangia Mawazo katika eneo la uwekezaji, Katibu Tawala wa Wilaya ya Sikonge Ndg. Andrea Ng'hwani amesema Sikonge bado tunahitaji kuongeza nguvu katika eneo la uwekezaji kwa sababu furasa bado zipo nyingi.



Naye Katibu wa baraza la Biashara Wilaya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sikonge Ndg. Selemani Pandawe amesema Sikonge bado ina fursa nyingi katika eneo la uwekezaji hivyo wazawa wasisite kuwekeza kwa nguvu hasa katika Ujenzi wa Shule,Hospitali Pamoja na eneo la Usafirishaji.

Akifunga baraza hilo Mhe. Chacha amewasihi wanachi kulichukulia maanani suala la uwekezaji " Naomba sana suala la uwekezaji tulizingatie,fursa zipo.Tusiogope kuthubutu,tutafakari,tusichelee kuwekeza Sikonge" amesema DC Chacha.



# KAMATI YA LISHE YAFANYA KIKAO CHA KUJADILI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA KAZI ZA AFYA NA LISHE KWA ROBO YA KWANZA (JULAI – SEPTEMBA 2023) KWA NGAZI YA KATA NA KIJIJI.

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge

Kamati ya Lishe ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge imeketi leo Novemba 3, 2023 katika kikao cha kawaida cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2023.

Akifungua kikao hicho Kaimu Katibu Tawala wa Wilaya ya Sikonge Bi. Faraja Hebel ametoa rai kwa Wajumbe kuendelea kutekeleza maagizo ya Serikali kuhusu afua za lishe ambapo Wilaya ikifanya vizuri Mkoa mzima wa Tabora utakuwa umefanya vizuri.

Kwa upande wake Afisa Lishe Wilaya Bi. Veronica Ferdinand akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa kazi za Afya na lishe amesema hali ya unyonyeshaji wa maziwa ya mama pekee ni nzuri kwa asilimia 93% na bado wanaendelea kutoa elimu juu ya unyonyeshaji sahihi na elimu ya lishe katika kata mbalimbali na katika vituo vya afya Wilayani Sikonge.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Ndg. Seleman Pandawe akichangia mjadala wa Taarifa ya Utekelezaji wa afua za afya wilaya amesisitiza juu ya kusimamia kikamilifu suala la kutoa chakula shuleni kwani kwa kufanya hivyo watakuwa wanatekeleza maagizo ya serikali na kutoa huduma yenye tija kwa wananchi.

Akifunga kikao hicho Mwenyekiti wa kamati hiyo ameagiza watendaji wa kata Kwenda kusimamia na kutekeleza mkataba wa lishe katika maeneo yao kwa ushirikiano mkubwa.





# MHE. MAGOPE AONGOZA BARAZA LA KAWAIDA LA WAHESHIMIWA MADIWANI KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI SIKONGE.

Na. Robert Magaka - Sikonge.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mhe. Rashid Magope aongoza baraza la kawaida la waheshimiwa madiwani leo tarehe 8 Novemba 2023.
Akifungua baraza hilo ameagiza wataalam kuongeza kasi ya ukusanyaji mapato na wale wachache wanaofanya kazi kwa mazoea waache mara moja.

Akitoa salamu za Mkoa kwa niaba ya kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Tabora Bw. Elihuruma Nyella ameipongeza Wilaya ya Sikonge kwa mapokezi mazuri ya Mwenge wa Uhuru na amesisitiza wataalam waendelee kuchapa kazi kwa bidi kwani kufanikiwa kwa Wilaya ya mkoa wa Tabora ni kufanikiwa kwa mkoa wa Tabora.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Ndg. Seleman Pandawe amepokea maelekezo na ushauri uliotolewa na Waheshimiwa Madiwani na ameahidi kuufanyia kazi kwa mujibu na taratibu za kiutumishi.

Aidha Mhe. Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Sikonge Bi. Anna Chambala amesisitiza kuimarisha ushirikiano baina ya chama na serikali kwani italeta tija katika kuwatumikia wanachi kwa ufanisi.

Akifunga kikao hicho Mhe. Rashid Magope Amemshukuru Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyopambana kuleta fedha nyingi za miradi ya maendeleo nchini kote na hususani Bilioni 1.3 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.



# DKT. CHRISTOPHER NYALU AONGOZA KIKAO CHA ROBO YA KWANZA CHA KAMATI YA LISHE JULAI HADI SEPTEMBA 2023 KATIKA UKUMBI WA HOSPITALI YA WILAYA SIKONGE.

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge.

Kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Dkt. Christopher Nyalu Mkuu wa Divisheni ya Afya Ustawi wa Jamii na Lishe ameongoza kikao cha Kamati ya Lishe kwa robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2023 katika ukumbi wa Hospitali ya Wilaya ya Sikonge.

Akiwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa afua za lishe kwa robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2023, Afisa Lishe Wilaya Bi. Veronica Ferdinand amesema katika utekelezaji wa robo hii ya kwanza viashiria vyote vya lishe vimetekelezwa vizuri kwa Zaidi ya asilimia themanini na kufikia rangi ya kijani isipokuwa kiashiria kimoja tu cha utekelezaji wa siku ya afya na lishe ya Kijiji au mtaa ambayo imetekelezwa kwa asilimia 71.8 na kufikia rangi ya njano ambayo ni kiashiria cha wastani.

Naye Mwenyekiti wa kikao Dkt. Nyalu akifunga kikao hicho amewashukuru wajumbe wote kwa michango yao yenye tija kwa kamati na ameelekeza kufanya kazi kwa ushirikiano ili kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa udumavu unaosababishwa na lishe duni wilayani Sikonge na Taifa kwa ujumla.





# "TUKATEKELEZE WAJIBU WETU KWA WELEDI HASA KATIKA KUSIMAMIA UJENZI WA VYOO BORA BILA KUPENDELEA WALA KUONEA MTU" MHE.DC CHACHA.

Na. Robert Magaka - Sikonge.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. Simon Chacha ameyasema hayo leo Novemba 10,2023 katika kikao cha kamati ya Afya ya Msingi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2023/24 katika Ukumbi wa Hospitali ya Wilaya ya Sikonge.

Akifungua kikao hicho Mhe. Chacha amesisitiza kufanya kazi kwa bidi na weledi ili kufikia malengo ya serikali ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

Aidha wakiwasilisha Taarifa za utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Idara ya Afya ya Msingi pamoja na mazingira wataalamu toka vitengo mbalimbali vya afya wameeleza jinsi shughuli hizo zinavyotekelezwa ikiwemo Idara ya Chanjo,Lishe na Afya ya Uzazi .

Taarifa imeonesha kuongezeka kwa idadi ya akinamama wajawazito wanaojifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na mwitikio mkubwa wa wananchi katika kupata chanjo mbalimbali kama vile surua,polio pamoja na chanjo mpya ya saratani ya shingo ya kizazi.
Kwa upande wake Mkuu wa Divisheni ya Afya,Ustawi wa Jamii na Lishe Dkt. Christopher Nyalu amemshukuru Mhe. Chacha na kuahidi kuyafanyia kazi yale yote yaliyoshauriwa na wajumbe wa kikao.
Akifunga kikao hicho Mhe. DC amesisitiza upandaji wa miti ya matunda hususani miche ya Miembe katika maeneo ya Chuo cha Maendeleo ya Wananchi (FDC), eneo la Kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki pamoja na Barabara ya bomani.



# "RC. BALOZI DKT. BURIAN ATEMBELEA WILAYA YA SIKONGE KUSIKILIZA NA KUTATUA KERO ZA WAKULIMA WA TUMBAKU KATA YA KISANGA.

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Balozi Dkt. Batilda Burian amezuru Wilayani Sikonge akiongozana na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa kusikiliza na kutatua kero za Wakulima wa Tumbaku hususani katika Kata ya Kisanga.

Akifungua kikao hicho Mhe. Balozi Burian amesema kilichosababisha kuja Sikonge ni baada ya kujitokeza kwa sintofahamu katika Chama cha Amcos Kisanga hasa baada ya kuuza tumbaku yao na wakulima kushindwa kupokea malipo ya jasho lao kwa sababu ya deni linalowakabili katika benki ya NMB Sikonge.

Mhe.Burian amesikitishwa sana na mwenendo wa kilimo cha tumbaku Sikonge hasa baada ya kuona jinsi wakulima walivyojituma kwa juhudi na kuishia kulipa madeni tu.

Akiongoza kikao hicho kilichohudhuriwa na wakulima pamoja na viongozi wao amesema haki ya wale waliolima lazima ipatikane “Hatuwezi kuwavumilia watu wanao wadhulumu wakulima” amesema Balozi Batilda.





Kwa upande wao wakulima wakiwasilisha malalamiko yao mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama Mkoa wa Tabora wamesema Chama cha Msingi Amcos Kisanga hakijawalipa wakulima haki yao na hii inasababishwa na kuwa na deni kubwa benki wanakochukua ruzuku,lakini pia kuna wakulima wasio waaminifu wanaochukua ruzuku lakini baada ya kuvuna tumbaku hukimbilia kuuza tumbaku soko huria hivyo kusabisha deni kubwa la fidia ya ruzuku kwa wakulima waaminifu.

Aidha imebainika kuwa viongozi wa chama cha msingi Amcos Kisanga kutumia madaraka yao vibaya kwa kushiriki kuuza tumbaku nje ya chama cha msingi lakini pia kushidwa kuwasomea deni wanalodaiwa wakulima katika chama cha Amcos Kisanga.

Baada ya kuwasikiliza wakulima na changamoto zao Mhe. Mkuu wa Mkoa aliahirisha kikao na kuamuru mara moja kuketi kama kamati ya uchunguzi ya mkoa ili kuleta suluhu ya kero zinazowakabili wakulima hao.

Baada ya kamati ya uchunguzi kuketi Zaidi ya masaa Matano ikiongozwa na Mhe. Dkt. Burian imebaini mambo Matano,Utoroshaji mkubwa wa tumbaku ili kukwepa kulipa deni la chama cha msingi,Changamoto katika chama cha Kisanga Amcos,imebaninika kumekuwa na utakatishaji mkubwa wa fedha,Ukopeshaji wa pembejeo wenye upendeleo,Utoaji mikopo wenye upendeleo,utoaji wa pembejeo usiozingatia uwezo wa mkulima,Udhaifu katika usimamizi wa tumbaku toka kwa Afisa ushirika na matumizi mabaya ya madaraka hasa katika kufanya maamuzi mbalimbali.

Akifunga kikao hicho Dkt. Burian ameamuru watumishi watano wanaohusika na masuala ya chama cha msingi Amcos na ushirika kuwekwa chini ya ulinzi ili kusaidia uchunguzi wa kero zilizobainika.



# SERIKALI YATENGA HEKTA 2500 ZA ARDHI KUGAWIA WANANCHI WANAOPISHA ENEO LA HIFADHI NYAHUA.

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. Simon Chacha ametembelea kata ya Nyahua akiambatana na Maafisa toka Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Tabora,Wakala wa Huduma za Misitu Kanda ya Magharibi,Wakala wa Huduma za Misitu Sikonge,Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge,Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge na wataalam wake,Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya pamoja na viongozi wa Chama Wilaya ya Sikonge.

Katika ziara hiyo Mhe. Chacha ameongea na Wananchi wanaoishi kwenye eneo la hifadhi katika vitongoji vya Luseseko,Manyanya na Kawemimbi.

Akiongea katika Mikutano ya hadhara kwenye vitongoji hivyo Mhe. Chacha amewasilisha Salamu za Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kwamba kwa busara na utashi wa Mheshimiwa Rais wananchi wote waliovamia eneo la hifadhi hawataondolewa kama ilivyokusudiwa awali bila kupatiwa eneo lingine la kuishi ili kupisha eneo hilo la hifadhi.

Aidha ameongeza kuwa wapo wataalam toka ofisi ya Kamishna wa Ardhi Mkoa wa Tabora watakao kwenda kushirikiana na viongozi toka kila kitongoji ili kuona na kupima eneo watakalohamia,hivyo wananchi wameombwa kutoa ushirikiano kwa wataalam hao pindi watakapofika kuanza zoezi hilo.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Sikonge Mhe. Anna Chambala amewasihi wananchi wanaoishi eneo la hifadhi kuwa zoezi litakapokamilika la kuwagawia eneo lingine wasijaribu tena kurudi na kuishi kwenye eneo la hifadhi kwani sheria itafuata mkondo wake.

Kwa upande wao wananchi wa vitongoji vya Luseseko,Manyanya na Mawemimbi wamemshukuru sana Mhe. Rais kwa kuwahurumia na kuamuru wapatiwe eneo lingine la kuishi nje ya eneo la hifadhi.





# MHE. CHACHA AZINDUA ZOEZI LA UGAWAJI WA VYANDARUA KWENYE KAYA KATIKA VIWANJA VYA TASAF SIKONGE.

Na. Robert Magaka - Sikonge.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. Simon Chacha amezindua zoezi la ugawaji wa vyandarua kwenye kaya katika viwanja vya Tasaf.

Akitoa salamu kwa niaba ya Mkurugenzi wa Bohari ya Dawa,Kaimu Meneja wa TRC Tabora Bw. Adonizedeki Tefurukwa amewashukuru wafadhili hususani Mfuko wa dunia kwa maendeleo kwa kuendelea kutoa mchango wake katika sekta ya afya hasa katika kupambana na Kifua Kikuu,Ukimwi pamoja na Malaria.Vilevile amewaomba wananchi kuzingatia matumizi sahihi ya vyandarua watakavyo gawiwa leo.

Mhe. Chacha akiwahutubia wananchi waliojitokeza kumsikiliza amesema takwimu zinaonesha kuwa Mkoa wa Tabora pamoja na Wilaya ya Sikonge unaongoza kwa maambukizi ya ugonjwa wa malaria hivyo lazima wananchi waelewe kuwa hali ni mbaya na lazima hatua za kupambana na malaria zichukuliwe ikiwa ni pamoja na kufanya usafi katika mazingira yetu pamoja na kuzingatia matumizi sahihi ya vyandarua.

Naye Kaimu Mkuu wa Divisheni ya Afya,Ustawi wa Jamii na Lishe Bi. Grace Mburi amesema hadi sasa Halmashauri imeandikisha kaya 44,225 kati ya kaya 56,735 zilizotarajiwa ambayo ni sawa na watu 360,909 kati ya watu 340,409 waliotarajiwa.

Vilevile amesema serikali imejipanga kuangamiza mazalia ya mbu kwa kuhakikisha kila kituo cha afya kinatenga fedha kwa ajili ya kununulia viuadudu kwa mwaka wa fedha ujao hasa katika maeneo sugu yanayotunza mazalia ya mbu.




Akitoa salamu za Halmashauri Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Sikonge Ndugu Seleman Pandawe amewasihi pia wananchi kufanya usafi wa mazingira katika maeneo yao ili kuangamiza mazalia ya mbu waenezao malaria na kutumia chandarua kujikinga na ugonjwa hatari wa malaria.

Zoezi hili linaendelea katika kata zote Wilayani Sikonge kupitia vituo 89 vya kupokelea vyandarua vilivyotengwa.





## “NATOA WITO KWA WATU WOTE HASA WANAUME KUJITOKEZA KUPIMA NA KUJUA HALI ZETU NA KUANZA KUTUMIA DAWA MAPEMA” MHE. CHACHA.

Na. Robert Magaka , Sikonge - Tabora.

Kauli hiyo imetolewa leo na Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. Simon Chacha alipokuwa akihutubia wananchi waliohudhuria maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

Aidha Mhe. Chacha amewasihi wananchi kuitikia wito wa kauli mbiu ya Siku ya Ukimwi duniani unaosema “Jamii iongoze kutokomeza Ukimwi” kwa kujitokeza kwa hiyari kupima virusi vya Ukimwi na kuanza kutumia dawa mapema kwa wale watakao bainika kuwa na maambukizi.

Akitoa Salamu za Chama, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Sikonge Bi. Anna Chambala ameutaka umma kuendelea kuongoza mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa kuelimisha jamii na kuwalinda vijana dhidi ya kila tabia hatarishi inayoweza kusababisha maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Mhe. Rashid Magope amewashukuru wananchi kwa juhudi zao na uelewa wao juu ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi hata kupelekea maambukizi ya virusi vya Ukimwi kupungua kiasi wilayani Sikonge kama takwimu zinavyo onesha mwaka 2023 maambukizi ni asilimia 1.5 ukilinganisha na takwimu za mwaka uliopita 2022 ambapo maambukizi yalikuwa asilimia 1.7.

Naye Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Bi. Kalista Maina amewasihi wananchi kuendelea kuwa na hofu ya Mungu na kuendelea kuwa waaminifu kwa wale walio katika ndoa ili kujikinga na maambukizi ya virusi vya Ukimwi nchini.



Akiwasilisha Taarifa ya Siku ya Ukimwi Duniani Bi. Haikael Mjema amesema serikali inaendelea na mapambano dhidi ya maambukizi ya Virusi vya Ukimwi na Ukimwi ikiwa ni pamoja na kusaidia kuunda vikundi 42 vya watu wanaoishi na virusi vya ukimwi,Kuendelea kutoa elimu ya ufahamu juu ya matumizi ya sahihi ya dawa za kufubaza makali ya virusi vya Ukimwi,Kuunda klabu tano za Watoto wanaoishi na virusi vya Ukimwi,kuendelea kuwa na vituo ishirini na moja vya kutolea dawa za kupunguza makali ya virusi vya Ukimwi pamoja na Upatikanaji wa dawa za kufubaza makali ya Virusi vya Ukimwi katika vituo vyote vya kutolea huduma sambamba na upatikanaji wa kondomu (mipira ya kiume) kwa mwaka mzima.



Akihitimisha maadhimisho hayo Mhe. Chacha amewashukuru wadau wote walio mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi ikiwa ni pamoja na MDH, IDT, CSSC, NACOPHA na COMPASSION Tanzania.

KAULI MBIU YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI

**“Jamii iongoze Kutokomeza Ukimwi”**




# MHE. NAIBU WAZIRI KIGAHE AZINDUA KIWANDA CHA KATI CHA KUCHAKATA NA KUFUNGASHA MAZAO YA NYUKI SIKONGE.

Na. Robert Magaka,Sikonge - Tabora.

Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara Mhe. Exaud Silaoneka Kigahe (Mb) amezindua leo Kiwanda cha Kati cha Kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki Sikonge.

Akihutubia wananchi waliohudhuria hafla hiyo Mhe. Kigahe ameupongeza Mkoa wa Tabora na Wilaya ya Sikonge kwa kufanikisha kujenga kiwanda cha Kuchakata na kufungasha mazao ya nyuki kwani ni kielelezo cha maendeleo ya viwanda nchini na tija kwa wafugaji wa nyuki ambao hapo awali walikuwa wakipata tabu ya soko la uhakika la bidhaa zao.

Aidha amebainisha changamoto za wafugaji wa nyuki ikiwepo ukosefu wa soko la uhakika,matumizi ya mizinga isiyo na kiwango inayopunguza uzalishaji wa asali pamoja na uvamizi wa wakulima na wafugaji katika maeneo ya hifadhi ambapo mizinga hutundikwa hivyo kusababisha nyuki kutoweka na hiyo kuleteleza uzalishaji wa asali kuendelea kuwa duni au kukosekana kabisa.

Hata hivyo Mhe. Kigahe amewahakikishia wananchi wa sikonge kuwa mfumo wa stakabadhi ghalani utasaidia sana kukomesha walanguzi wanao nunua asali kwa bei ya chini isiyoleta tija kwa wafugaji.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Dkt. Batilda Salha Burian ametoa wito kwa wafugaji wa nyuki na wananchi kwa ujumla kuifanya biashara ya mazao yatokanayo na nyuki kuwa mahususi kama nchi zingine zinavyofanya ingawaje zinazalisha asali kwa kiasi kidogo kuliko sisi.

Akitoa Taarifa ya Ujenzi wa Kiwanda hicho ,Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge Ndg. Seleman Pandawe amesema serikali itaendelea kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakao ingia kwenye hifadhi za misitu bila kufuata utaratibu uliowekwa ili kudhibiti uhalibifu wa mazingira pamoja na kulinda biashara ya ufugaji nyuki ambao unategemea sana mazingira haya ya hifadhini.



Kwa upande wao wananchi wa Sikonge waliojitokeza katika tukio hili muhimu wamesema wanaishukuru sana serikali ya awamu ya sita kwa kutekeleza maana ya maendeleo kwa vitendo kwa kuwajengea kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki kwani kitazalisha ajira na kuwasaidia wanachi kuuza asali yao kwa bei yenye tija,ombi lao kwa serikali nikuruhisiwa kuingia na pikipiki kwenye hifadhi wakati wa msimu wa kuvuna asali ili irahisishe shughuli za kubeba mazao yao ukilinganisha na jinsi wanavyotumia baiskeli kwa sasa.





# MHE. CHACHA AONGOZA KIKAO CHA KAMATI YA USHAURI WILAYA YA SIKONGE (DCC).

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge.

Mkuu wa Wilaya ya Sikonge Mhe. Simon Chacha ameongoza kikao cha kamati ya ushauri Wilaya ya Sikonge kilichofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

Akichangia hoja ya uzalishaji katika ngazi ya Wilaya Mhe. Chacha amesema lazima tutumie teknokojia ya kisasa katika uzalishaji wetu ili eneo dogo litoe uzalishaji mkubwa.

Akiwasilisha utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Wilaya ya Sikonge Bi. Mkesika Mageta ambaye ni Afisa Mipango amesema Serikali itaendelea kutoa elimu bila malipo kwa nchi nzima ikiwemo Sikonge.

Wajumbe walio hudhuria kikao hicho wameipokea Taarifa ya utekelezaji wa Shughuli mbali mbali za kisekta kwa moyo mmoja na kushauri kuwa Taarifa ya utekelezaji isisahau kueleza na changamoto pia inazokabiliana nazo katika kutekeleza shughuli za maendeleo.



Akufunga kikao hicho Mhe. Chacha amewataka Wataalam kuboresha Taarifa yao kwa kuongeza kipengele cha changamoto wanazokumbana nazo katika kutekeleza shughuli za maendeleo “Msieleze tu mafanikio muweke wazi na changamoto zinazokabili sekta husika na kwa kupitia kikao hiki wajumbe wataona washaurije ili tusonge mbele” amesema Mhe. Chacha.




# KAMATI YA SIASA WILAYA YA SIKONGE IMEPOKEA NA KURIDHIA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM KWA KIPINDI CHA JULAI HADI DESEMBA ,2023.

Na. Mwandishi Wetu - Sikonge.

Akitoa Taarifa ya utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Simon Chacha ameelezea kwa kina juu ya mambo yaliyotekelezwa katika sekta ya Kilimo na Mifugo,Elimu,Miundombinu,Afya,Mazingira,Mawasiliano pamoja na Ulinzi na Usalama.

Mbali na Serikali kuendelea kuwahudumia wananchi kupitia wataalam katika sekta mbalimbali imebainika kuwa bado kuna changamoto zinazokwamisha utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa ufanisi ikiwa moja ya changamoto hizo ni uhaba wa watumishi katika sekta mbalimbali, hata hivyo Mhe. Chacha ameeleza jinsi Serikali ya Wilaya inavyopambana kuhakikisha changamoto hiyo inakoma,"ipo mikakati ya kuomba kibali cha ajira ili kuweza kuziba pengo hili la uhaba wa watumishi,kuendelea kuwabadilishia kada watumishi waliojiendeleza katika fani zingine" amenena Mhe. Chacha.

Aidha Mhe. Joseph George Kakunda,Mbunge wa Jimbo la Sikonge akitoa salamu kwa kamati ya Siasa Wilaya amewaomba wajumbe kuwa tayari kuisadia serikali hasa katika maeneo ambayo miradi ya maendeleo inatekelezwa ikiwa ni kwa kuuunga mkono miradi hiyo na wala sio kukwamisha.

# NUKUU MBALIMBALI ZA VIONGOZI

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM KWA KAMATI YA SIASA WILAYA KWA KIPINDI CHA MWEZI JULAI HADI DESEMBA, 2023.**



"Katika Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM changamoto ni pamoja na uhaba wa Watumishi katika sekta mbalimbali.

Hata hivyo Serikali inaendelea kuomba nafasi hizo kujazwa kwa kupanga bajeti ya mishahara kwa ajili ya kuajiri watumishi wapya.

**MHE. SIMON CHACHA**
Mkuu wa Wilaya ya Sikonge

www.sikongedc.go.tz ded@sikongedc.go.tz sikongedc

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

**YALIYOJILI KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA UKIMWI DUNIANI - DISEMBA 1, 2023**



"Naomba nitoe wito kwa wadau wa ndani na nje kwamba endeleeni kutoa michango yenu kwa nia njema ya kuokoa maisha ya wanasikonge na watanzania wenzetu. Tunapotekeleza mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI hatuwezi kuacha kuhamasisha jamii hasa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya ambazo zinachangia maambukizi.Yakitumika humfanya mtu kupoteza ufahamu na hivyo hujihusisha na matendo ya ngono,kujidunga sindano na mengineyo.

**Mhe. Simon Chacha**
Mkuu wa Wilaya ya Sikonge

www.sikongedc.go.tz ded@sikongedc.go.tz sikongedc

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

**KIKAO CHA KAMATI YA LISHE : ROBO YA KWANZA JULAI - SEPTEMBA 2023.**

"Hakikisheni watoto wote wanapata chakula shuleni,huko shuleni kuna yatima,watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu.Ili mtoto asione kwenda shule ni adhabu katika maisha yake.

Kwa namna yoyote ile lazima tuweke mkazo katika eneo la watoto kupata chakula shuleni na hiyo ndio kazi yetu viongozi."

**Novemba 3, 2023**



**NDG. SELEMAN PANDAWE**
Mkurugenzi Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

www.sikongedc.go.tz ded@sikongedc.go.tz sikongedc

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

**MAADHIMISHO YA MIAKA 62 YA UHURU WA TANZANIA BARA - DISEMBA 9, 2023.**

"Umoja na Mshikamano ni chachu ya Maendeleo ya Taifa Letu"

MIAKA 62 YA UHURU

Mwalimu Nyerere aliwahi kuzungumza na Waandishi wa Habari akawaambia kusudi lake halikuwa kuunda jamii ya watu wasio weza kuhoji mambo, nasi pia tuzingatie hilo kwa vijana wetu, hasa hawa wanafunzi.

Kuwa na Mawazo tofauti na wengine sio kosa kama ipo hoja ya msingi, kuwa na vijana wanaosifia kila kitu bila kuhoji kwa namna hiyo hatuwezi kutengeneza taifa lenye fikra tunduizi.



**Mhe. Simon Chacha**
Mkuu wa Wilaya ya Sikonge

www.sikongedc.go.tz ded@sikongedc.go.tz sikongedc



© **HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE -2024.**

S.L.P 70 SIKONGE - TABORA.

SIMU: **+255 767 135 460 / +255 753 795 030**

www.sikongedc.go.tz

ded@sikongedc.go.tz

@sikongedc

Sikonge DC TV